

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA

SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO

Reg. No. S.576

Simu: 0762818180/0754636049/0621064022

Tovuti: www.ruhuwikoschools.ac.tz

Barua pepe: ruhuwikosecschool@gmail.com



S.L.P. 448.

SONGEA.

Tarehe:

JINA LA MWANAFUNZI:

YAH: **MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS) KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO 2026 / 2027**

1.0 **UTANGULIZI**

Shule ya Sekondari Ruhuwiko ni miongoni mwa Shule kumi zinazomilikiwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). Shule hii ipo Songea Mjini Mkoa wa Ruvuma katika eneo la Kikosi cha Jeshi (411 KJ) barabara iendayo Wilaya ya Mbinga. Hivyo napenda kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Ruhuwiko Kidato cha **TANO** Mwaka 2026/2027. **Shule itafunguliwa Tarehe 06/07/2026**. Kutakuwa na masomo ya awali (**Pre Form Five**) kwa anayehitaji kuanzia Mwezi **Februari 2026** hadi **05/06/2026** kwa wanafunzi wenye sifa za kujiunga na kidato cha tano ambao watapenda kuanza mapema kabla ya muda wa kufungua Shule rasmi. Masomo hayo yanachangiwa gharama zifuatazo ambazo zinalipwa Benki kwa Awamu moja.

BWENI	KUTWA
Tshs. 400,000/=	Tshs. 200,000/=

2.0 **NAMNA YA KUJISAJILI**

Ufikapo shuleni unatakiwa kuripoti Ofisi ya Usajili ukiwa na **Fomu ya Maombi**, **Picha moja** (Passport), Nakala ya **Cheti Cha Kumaliza Kidato Cha Nne** au **Cheti cha Matokeo ya Kidato cha Nne (Result Slip)** na nakala ya **Cheti cha Kuzaliwa**.

3.0 **MALIPO YA ADA KUANZIA MWEZI JULAI**

ADA YA BWENI		ADA YA KUTWA	
JULAI	- TSHS. 450,000/=	JULAI	- TSHS. 325,000/=
SEPTEMBER	- TSHS. 450,000/=	SEPTEMBER	- TSHS. 325,000/=
JANUARI	- TSHS. 450,000/=	JANUARI	- TSHS. 325,000/=
APRILI	- TSHS. 450,000/=	APRILI	- TSHS. 325,000/=
KWA MWAKA = TSHS. 1,800,000/=		KWA MWAKA = TSHS. 1,300,000/=	

ZINGATIA: ADA IKILIPWA HAITARUDISHWA

Malipo ya ada ya shule yalipwe kupitia benki tu kwenye **A/C No. 023101000790 NBC**, **A/C No. 01J1085291000 CRDB** au **A/C No. 61803500130 NMB** jina la akaunti ni **MKUU WA SHULE RUHUWIKO SEKONDARI** na "Original Pay in Slip" iletwe Shuleni Ofisi ya Ada. Kumbuka kuandika Majina ya Mwanafunzi kwenye risiti ya Benki wakati wa kulipa Ada. Hakuna malipo ya fedha za Ada yanayopokelewa taslimu shuleni, isipokuwa fedha za Sare, Bima, Kitambulisho, Kitini, Nembo, Jembe na Kwanja ziletwe Taslimu (Cash).

4.0 **UKARABATI WA MIUNDOMBINU**

Kutakuwepo na mchango wa ukarabati wa miundombinu ambapo kila mwanafunzi anayesoma shule hii anatakiwa kuchangia ili kuweza ukarabati miundombinu inayoharibika au kupata hitilafu kwa kuwa inatumika mara kwa mara. Kwa mwaka huu mchango huo ni **Tshs. 60,000/=** ambapo kiasi hicho kinaweza kulipwa kwa awamu mbili yaani **muhula wa kwanza Tshs. 30,000/=** na kumaliza kiasi hicho hicho **muhula wa pili**. Kwa wanaoweza wanaruhusiwa kulipa kiasi chote kwa mwaka mzima. **Mchango huu ulipwe Benki kupitia akaunti za Shule zilizotajwa hapo juu.**

5.0 **(A) SARE ZA SHULE (UNIFORMS)**

Mwanafunzi **haruhusiwi** kujishonea Sare za Shule. Sare zote zinashonwa shuleni ili kuleta mfanano wa rangi ya vitambaa na namna ya ushonaji ambayo ni ya mavazi yenye maadili kwa wanafunzi na kwa jamii kwa ujumla. **Mwanafunzi wa Bweni** (Mvulana/Msichana) atashonewa Suruali mbili/Sketi mbili, Nguo ya kuvaa baada ya muda wa Masomo (Shamba Dress), Tai na atapatiwa Sweta lenye nembo na T-shirt yenye nembo kwa gharama ya **Tshs. 150,000/=** na **Mwanafunzi wa Kutwa** (Mvulana/Msichana) atashonewa Suruali mbili/Sketi mbili, Tai na atapatiwa Sweta lenye nembo na T-shirt yenye nembo kwa gharama ya **Tshs. 110,000/=**. Fedha za Sare ziletwe **Taslimu (Cash)** Shuleni Ofisi ya Mhasibu siku ya Kuripoti.

(B) Mzazi/mlezi mnunulie mwanao:-

- i. Tracksuit pea 2 rangi ya bluu iliyokolea, Fulana (Jezi) pea 2 ya rangi ya bluu iliyokolea na Raba ya Rangi Nyeupe (***Wakati wa Kuripoti Unatakiwa Kuvaa Track Suit, Jezi na Raba ulizoelekezwa***)
- ii. Viatu vyeusi vya Kamba, Mashati mawili meupe ya mikono mifupi.
- iii. Soksi nyeusi na mkanda mweusi kwa mvulana na soksi nyeupe kwa msichana.

(C) MICHANGO MINGINE

- i. Nembo mbili za kushonea kwenye Mashati ya Shule = **Tsh. 10,000/=** iletwe Taslimu (Cash).
- ii. Kitambulisho cha Shule kitatengenezwa kwa gharama ya **Tsh. 10,000/=** iletwe Taslimu (Cash).
- iii. Kitini (Summary Book) – kinapatikana shuleni kwa **Tsh. 18,000/=** iletwe Taslimu (Cash).

6.0. HUDUMA YA AFYA

Kila Mwanafunzi anatakiwa kuja na **Bima ya Afya** na kwa yule ambaye hana anatakiwa kuja na **Fedha Taslimu (Cash) Tshs. 50,400/=** kwa ajili ya kukatiwa bima ya Afya.

7.0. GHARAMA ZA MAFUNZO KWA VITENDO (PRACTICAL)

Kwa mwanafunzi anayesoma Tahasusi (Combination) ya Sayansi anatakiwa kuchangia gharama za mafunzo kwa vitendo ili kumwezesha kufaulu vizuri masomo yake ya Sayansi. Gharama hizo ni **Tshs. 100,000/= kwa mwaka au Tshs. 50,000/= kila nusu Muhula**. Lipa kupitia Benki ya Posta Akaunti namba (**TCB 300207000220** – Jina la Akaunti ni Mkuu wa Shule Ruhuwiko Sekondari).

8.0. VIFAA VYA DARASANI NA MAZINGIRA

- a. Kamusi kubwa (English – English Oxford Dictionary)
- b. Daftari kubwa (*Counter Books*) – idadi kulingana na masomo unayosoma.
- c. Vitabu vya Masomo (**Orodha ya Vitabu Imebambanishwa na ni Muhimu kuwa navyo**).
- d. Rimu **bunda mbili** muhula wa kwanza anaporipoti na **bunda moja** muhula wa pili.
- e. Fagio la mpira la kudekia – mopa (*Rubber squeeze*) –1.
- f. Ndoo moja ya plastiki ya lita 20, Ufagio wa Chelewa -1.
- g. Brashi ngumu fupi 1 na Fagio laini ndefu 1.
- h. Jembe lenye mpini - 1
- i. Kwanja - 1
- j. Kila mwanafunzi awe na **Saa ya mkononi** na Kitambaa (**Leso**) nyeupe.

9.0. VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI WA BWENI

- a. Godoro la futi 2½, Shuka mbili rangi ya **Bluu bahari**, Blanketi 1, mto na Chandarua (net).
- b. Sanduku imara la chuma (Tranka) na Kufuli imara.
- c. Ndoo ya lita 10 ya kuogea, Taulo na Kandambili.
- d. Vyombo vya kulia Chakula (*Kontena, Kikombe na Kijiko*).
- e. Vitenge 2 kwa msichana na Vitu vidogovidogo kwa matumizi yake binafsi.

ZINGATIA: VIFAA NA MAHITAJI HAYO YANAPATIKANA DUKANI SHULENI ISIPOKUWA VITABU

10.0. NGUO MAALUMU ZA KUVAA BAADA YA VIPINDI (SHAMBA DRESS)

Mwanafunzi wa bweni anavaa nguo ya kazi baada ya muda wa masomo na siku zote ambazo sio za masomo (*weekend days*). Utaratibu huu ni **wa lazima** kwa kila mwanafunzi wa bweni ili kudumisha nidhamu, kuondoa vishawishi vya wizi wa mavazi ya nyumbani na tabia nyingine mbaya zinazoambatana na uvaaji wa nguo za nyumbani. Mvulana atashonewa na shule shati na suruali jozi moja na msichana atashonewa na shule gauni la heshima (refu). **Nguo za nyumbani haziruhusiwi** na ukaguzi unafanywa mara mwanafunzi anapofika Shuleni.

11.0 MAMBO MENGINE YA KUZINGATIA

- i. **Wastani wa Shule:-** Mwanafunzi anatakiwa kupata **wastani wa kuanzia 60%** na kuendelea katika masomo yake yote ili awe amefaulu mitihani ya ndani na kuendelea na Kidato cha Sita.
- ii. **Simu haziruhusiwi kabisa kwa Mwanafunzi:** Mwanafunzi atakayekamatwa na simu hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuchoma simu na mwanafunzi kusimamishwa Shule mara moja.
- iii. **Sheria za shule:-** Kila mwanafunzi atapewa nakala ya Sheria za Shule ambazo anatakiwa kuzifuata kikamilifu pamoja na taratibu nyingine atakazoelekezwa.

KARIBU SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO UPATE ELIMU BORA NA NIDHAMU THABITI.

[Signature]

THE HEADMASTER
RUHUWIKO SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 448
SONGEA, RUVUMA

MINISTRY OF DEFENCE AND NATIONAL SERVICE

RUHUWIKO SECONDARY SCHOOL



S.L.P 448, SONGEA

Owned By TPDF

Mob: 0762818180 / 0754636049 / 0621064022

Website: www.ruhuwikoschools.ac.tzEmail: ruhuwikosecschool@gmail.com

MEDICAL EXAMINATION FORM

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

TO MEDICAL OFFICER

.....

REF: Mr/Mrs/Miss:

Please examine the above named if he/she is physically and mentally fit for full time studies. The examination should include the following categories:

1. a. Eye sight
- b. Hearing
- c. Limbs
- d. Venereal disease
- e. Speech
- f. Leprosy
- g. Epilepsy
2. Neuroses
3. Pregnancy
4. Other serious disease (If any) Physical defects, impairment e.g. Legs, Arm etc, infection chronic or family disease etc

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

[To be completed by a Government Medical Officer]

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for full time studies.

Date: Signature:

Station: Designation

[Signature]
 THE HEADMASTER
 RUHUWIKO SECONDARY SCHOOL
 P.O.Box 448
 SONGEA, RUVUMA

RUHUWIKO HIGH SCHOOL

**TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION (TIE) - ADVANCED LEVEL BOOKS
FORM FIVE AND FORM SIX**

1. Orodha hii ya vitabu ni vitabu ambavyo vimeandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ambayo ni taasisi ya serikali iliyopewa majukumu ya kuandaa na kusambaza/kuuza vitabu vinavyotumika shuleni na hutumika kama vitabu maalumu vya kufundishia. Hivyo, mzazi/mlezi unashauriwa na unaombwa kumnunulia mwanao vitabu vya Taasisi ya Elimu Tanzania kwa masomo ambayo anasoma. Vitabu hivyo vinasaidia kujisomea ili kuendana na mitaala ya Elimu inayotolewa hapa Tanzania. Orodha ya vitabu hivyo ni ifuatavyo:-

- a. TIE (2022); *Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Five.
- b. TIE (2022); *Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Six.
- c. TIE (2019); *Basic Applied Mathematics for Advanced Level Secondary Schools*; Student' Book. Form Five and Six. Tanzania Institute of Education.
- d. TIE (2019); *Biology for Advanced Level Secondary Schools*; Student' Book. Form Five. Tanzania Institute of Education.
- e. TIE (2019); *Biology for Advanced Level Secondary Schools*; Student' Book. Form Six
- f. TIE (2019); *General Chemistry for Advanced Level Secondary Schools*; Student' Book. Form Five and Six.
- g. TIE (2019); *Physical Chemistry for Advanced Level Secondary Schools*; Student' Book. Form Five and Six.
- h. TIE (2019); *Organic Chemistry for Advanced Level Secondary Schools*; Student' Book. Form Five and Six
- i. TIE (2019); *Inorganic Chemistry for Advanced Level Secondary Schools*; Student' Book. Form Five and Six
- j. TET (2019); *Kiswahili – Fasihi Shule za Sekondari*; Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita.
- k. TET (2019); *Kiswahili– Lugha na Sarufi Shule za Sekondari*; Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita.
- l. TIE (2019); *Physics for Advanced Level Secondary Schools*; Student' Book. Form Five.
- m. TIE (2019); *Physics for Advanced Level Secondary Schools*; Student' Book. Form Six.
- n. TIE (2022); *English for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Five.
- o. TIE (2022); *English for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Six.
- p. TIE (2022); *History for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Five.
- q. TIE (2022); *History for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Six.
- r. TIE (2022); *Macroeconomics for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Five and Six.
- s. TIE (2022); *Microeconomics for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Five.
- t. TIE (2022); *Accountancy for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Five.
- u. TIE (2023); *Accountancy for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Six.
- v. TIE (2022); *Physical Geography for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Five and Six.
- w. TIE (2022); *Practical Geography for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Five and Six.
- x. TIE (2022); *Human Geography for Advanced Secondary Schools*; Student' Book. Form Five and Six.

SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO

2. Ndugu Mzazi/Mlezi, unaombwa kumnunulia mwanao vitabu vya ziada vya masomo ambayo anayasoma angalau kila somo kitabu kimoja. Lengo ni kuwapa uwezo wanafunzi kujisomea ili kuongeza maarifa darasani na kufaulu vizuri katika mitihani yao. Orodha ya vitabu vya ziada vinavyopendekezwa kwa kila somo ni kama ifuatavyo:-

ORODHA YA VITABU KIDATO CHA TANO NA SITA

a. ADVANCED MATHEMATICS

- i. Shayo. *Advanced Mathematics*
- ii. Tranter. *Advanced Mathematics*
- iii. Backhouse. *Advanced Mathematics*, Book 1 and 2.
- iv. Chand, S. *Advanced Mathematics 1 and 2*.
- v. Scandler & Thorning. *Understanding Pure Mathematics*
- vi. Chand, S. *Principles of Mathematics*, Class XII

b. PHYSICS

- i. Nelkon & Parker. *Advanced Level Physics*, 7th edition.
- ii. Chand, S. *Principles of Physics*. Class XI.
- iii. Chand, S. *Principles of Physics*. Class XII.
- iv. Breithaupt, J. *Understanding Physics*, 2nd / 4th edition.
- v. Monastery, R. *Advanced Level Physics* 4th edition.
- vi. Nelkon & Parker. *Physics*.
- vii. Thoncaster, R. *Physics*.
- viii. Duncan, T. *Advanced Level Physics*
- ix. *Calculations for Advanced Level Physics*.

c. CHEMISTRY

- i. Delungu. *Physical Chemistry*, (Mzumbe Bookshop Project, 1998)
- ii. Finar, I.L. *Organic Chemistry*, Part 1. The Fundamental Principles (Longman LTD)
- iii. Ramsden. *Chemistry*
- iv. Ramsden. *Advanced Chemistry*.
- v. Chand, S. *Principles of Chemistry*. Class XI & XII.

d. BIOLOGY

- i. *Biological Science BS*. Cambridge University Press, 1997 3rd edition.
- ii. Robert, M. *Fundamental Approach*.
- iii. Toole, S. *New Understanding Biology*.
- iv. Clege, C.J. & Muckean. *Advance Biology Principles and Application*.
- v. Kent, M. *Advanced Biology*; Oxford University Press - Uk
- vi. Glem & Susan, T. *Understanding Biology for Advanced Level*.
- vii. Glem & Suzan, T. *Advanced Understanding Biology*.

e. HISTORY

- i. Kato. A. *Mastering Advanced Level History*. History 2.
- ii. *Advanced Learners History*. Form V & VI (History 1 and 2) (By Oxford 2011)
- iii. TIE. *History for Secondary Schools*, History I- Form Five.
- iv. Kamili, Z. (2010). *Advanced level History for Africa From Neolithic Revolution to Present*
- v. *Major Events in the World History*.
- vi. Nyambari Nyangwine, (2007). *Advanced Level History*
- vii. Ponsian, J. (2012). *Focus on Modern world History*.
- viii. Shibiliti, CK. *Contemporary Historical Events*. History 1.

f. KISWAHILI

- i. Kiswahili I - *Nadharia ya Lugha*: Kidato cha Tano na Sita. Nyambari Nyangwine.
- ii. *Nadharia ya Fasihi na Uhakiki* - Masuko C. Saluhaya
- iii. *Nadharia ya Lugha Kidato cha V & VI na Elimu ya Juu* - Masuko C. Saluhaya
- iv. *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili* – Karanja, P. & Habwe, J.
- v. *Kitangulizi Cha Tafsiri* – Masuko, J.
- vi. *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili* - Waihiga, G.

g. ENGLISH LANGUAGE

- i. *Advanced Level English Language 1 Form 5 & 6* by S.G.N, J.E.Kinunda
- ii. Asheli, N. *Advanced Level English Practical Approach 2nd ED*
- iii. *Stylistics & Communication in English* by Simwamba M.A
- iv. Asheli, N. *Language One*.
- v. Kadege, M. *Language One*.
- vi. Asheli, N. *A Practical Approach*
- vii. *Oxford Advanced Learner's Dictionary*

h. GEOGRAPHY

- i. Monk FJ. *Principles of Physical Geography*.
- ii. Waugh, D. *Geography an Integrated Approach*.
- iii. Mwita, J. *Essentials of Practical Geography*.
- iv. Burnet, RB. *General Geography in Diagram*.
- v. Msabila, DT. *Simplified Physical Geography (A-Level)*
- vi. Gregory, S. *Statistical Methods and the Geographers*
- vii. Msabila, DT. *Human and Economic Geography*
- viii. Kamili, Z. *Physical Geography*.
- ix. Kamili, Z. *Human and Economic Geography*
- x. Write, R. *Africa in Focus* (Physical, Human and Economic).
- xi. Msabila, DT. *Comprehensive Approach to Physical Geography*
- xii. *Principles of Physical Geography – By Monkhouse*

i. ECONOMICS

- i. *An Introduction to Economic Theory* by Gupta, B.L 3rd Edition.
- ii. Gupta, B.L. *Economics Theory*
- iii. Dwivedi. *Micro-economics*
- iv. Saleemi, N.A. *Economic Simplified*
- v. Mudida. R. *Modern Economics*.
- vi. Dewett, K.K. *Modern Economy Theory*.

j. COMMERCE

- i. Masasi, S.J. (2009). *Certificate COMMERCE for form Five and Professional Business Studies* (New Syllabus Approach) - Paper 1. Stephens Commercial Publishers.
- ii. Masasi, S.J. (2009). *Certificate COMMERCE for form Six and Professional Business Studies* (New Syllabus Approach) – Paper 2. Stephens Commercial Publishers.

k. ACCOUNTANCY

- i. Frankwood. *Business Accounting 1 & 2*.
- ii. Manheshwari. *Advanced Accountancy*, Volume 1.

l. GENERAL STUDIES

- i. *Democracy and Development* by BHANGWATI J, N 2002
- ii. *The Concept and Theories Of Modern Democracy*
- iii. *Foreign Policy of Tanzania 1961-1981* by MATHEW, K &S. MUSHI
- iv. *Technology and Industrialization in Africa, DAKAR* by YASHIR F. (1987)
- v. Omari, CK. *Towards Rural Development in Tanzania*
- vi. Ishumi. *Philosophy of Education*.
- vii. Joanes, B. *Understanding Advanced Level General Studies*
- viii. *General Studies for A-Level Certificate Form V*
- ix. Nyambari, N. *Contemporary Approach for A-Level General Studies* Notes for Form V and VI.
- x. *General Studies Supplementary*. Book For A level and Colleges

m. BASIC APPLIED MATHEMATICS

- i. Kiza & Septine, I. *Basic Applied Mathematics*

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA
SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO

SHERIA ZA SHULE

UTANGULIZI

Sheria na taratibu za Shule zimewekwa ili zitumike kama mwongozo wa maisha na malezi bora kwa wanafunzi wanaohusika ili kuleta nidhamu inayofaa kwa kujifunza na pia jumuiya inayohusika iweze kuishi pamoja kwa amani na kushirikiana. Hivyo kila mwanafunzi aliyekubali kujiunga na Shule hii anawajibika kufuata sheria na taratibu za shule hii. Ikiwa wewe ni mwenye kuelewa wajibu wako kuwa **NIA YAKO KUBWA NI KUPATA ELIMU**, sheria na taratibu hizi utaziona nyepesi kufuata. Kuvunjwa kwa sheria na taratibu hizi kutachukuliwa kuwa ni utovu wa nidhamu na hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mvunjaji. Hivyo unapaswa kusoma na kuzielewa vizuri sheria zifuatazo:-

S/No.	AINA YA KOSA	UFAFANUZI WA KOSA	KIWANGO CHA ADHABU
1.	WIZI	a. Wizi wa mali za shule, wizi wa mali za mwalimu, mwanafunzi mwenzake, mtu yeyote nje au ndani ya shule. b. Mwanafunzi kukamatwa na karatasi yoyotendani ya chumba cha mtihani mbali na ile ya maswali/kujibia au kukamatwa akiongea au kuoneshana majibu na mwenzake. c. Kumfichia siri mwizi kwa kukataa kumtaja, kwa kuharibu ushahidi au kushirikiana na mwizi katika kutekeleza wizi huo.	Kufukuzwa shule. Kufutiwa mtihani unaohusika pamoja na mingine yote atakayokuwa amefanya. Kusimamishwa shule mara moja.
2.	UASHERATI	a. Uasherati, kukutwa na barua za mapenzi, kuwa na wapenzi ndani na nje ya shule, kukutwa na kondomu/vidonge vya kuzuia mimba, kupata mimba au kusababisha mimba. b. Kutoa mimba au kusaidia kitendo cha kutoa mimba.	Kufukuzwa shule mara moja. Kufukuzwa shule mara moja.
3.	ULEVI	a. Ulevi wa aina yoyote kwa mfano pombe na madawa ya kulevya. b. Kuonekana katika mabaa au nyumba za wageni (guest house).	Kufukuzwa shule maramoja. Mzazi/mlezi kuitwa shuleni na adhabu ya viboko.
4.	KOSA LA JINAI	a. Mwanafunzi yeyote atakayehusika na kosa la jinai b. Mwanafunzi yeyote atakayetiwa hatiani na mahakama.	Kufukuzwa shule mara moja. Kufukuzwa shule mara moja.

5.	KUPIGANA	a. Mwanafunzi atakayesababisha ugomvi b. Mwanafunzi aliyeanza kumpiga mwenzake au kumkodi mtu mwingine kutimiza lengo hilo.	Kufukuzwa shule mara moja. Viboko sita hadharani.
6.	KUHARIBU MALI YA UMMA	a. Kuharibu Mali ya umma, shule, mwalimu au mwanafunzi mwingine, kuinamisha seng'enge na kutoroka/kuingia shuleni.	Kusimamishwa shule siku 21.
7.	KUDHARAU, KUTUKANA NA KASHFA	a. Kumdharau, kumkashfu na kumtukana mwalimu au kiongozi. b. Kudharau amri halali zilizotolewa. c. Kudharau bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, fedha za nchi na viongozi wa serikali.	Kufukuzwa shule mara moja.
8.	KUOA AU KUOLEWA	a. Yeyote atakayegundulika kuwa ameo au ameolewa. b. Yeyote atakayegundulika kuwa ana mtoto.	Kufukuzwa shule mara moja.
9.	KUGOMA	a. Yeyote atakayedhibitishwa amegoma adhabu ya kiongozi au mwalimu. b. Kumkimbia mwalimu baada ya kukosa. c. Atakayegoma adhabu au kumtishia mwalimu au kumpiga kiongozi wake.	Atalazimishwa adhabu hiyo mbele ya wenzake. Atakayekubali atatekeleza ataongezewa kusimamishwa shule siku 21. Kosa b na c atafukuzwa shule.
10.	UTORO NA MAHUDHURIO HAFIFU	Siku moja ya utoro au kukosa shule, utoro uliokithiri zaidi ya siku 21, mwanafunzi wa bweni kulala nje ya shule bila kibali cha uongozi wa shule.	Viboko 4, kumwita mzazi na viboko 6 hadharani, kufukuzwa shule.
11.	TAALUMA	a. Kutohudhuria vipindi, kutoandika, kutofanya majaribio na kazi zozote za kitaaluma. b. Kutozungumza kiingereza. Kupata maksi chini ya asilimia 50% kwa kidato cha I hadi IV na asilimia 60% kwa kidato cha V na VI katika majaribio. c. Kupata maksi chini ya 50% kwa kidato cha 1 & 3 na chini ya 60% wa kidato cha 5 kama wastani wa mwaka kuweza kuendelea kidato kinachofuata.	Viboko visivyozi 6 kila kosa. Viboko visivyozi 6 kulingana na maksi mtu alizopata. Kutafuta shule nyingine au kurudia darasa aukusajiliwa kama mtahiniwa wa kujitegemea kwa kidato cha sita.
12.	KUCHELEWA	a. Yeyote anayechelewa na kufika baada ya 07:00 asubuhi. b. Yeyote anayechelewa kuingia darasani, kwenda mstarini, kuripoti anapoitwa au kufikanyumbani. c. Atakayechelewa kwenye chumba cha mtihani zaidi ya nusu saa.	Onyo kali na viboko 4. Hatafanya mtihani unaohusika.

13.	MIPAKA YA SHULE	a. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwepo pale anapostahili wakati wowote kufuatana na taratibu za shule. b. Ruhusa itatolewa na mwalimu pale mwanafunzi anapostahili kwenda sehemu nyingine. c. Sehemu zifuatazo ni nje na mipaka ya shule:- chumba cha walimu, ofisi ya shule, maabara ya hospitali, ofisi za kikosi na nyumba za kuishi kikosini. d. Ni marufuku kusimama bila sababu nje ya mlangowa kuingia shule.	Atakayeonekana nje ya mipaka ya shule viboko visivyozi 6
14.	SARE YA SHULE	a. Kuvaa sare isiyo ya shule b. Mshono usio wa heshima c. Kaptura au sketi fupi au ndefu mno d. Kutovaa necktie, strips au skai, nembo ya shule. e. Sare chafu au iliyochanika f. Kuvaa sketi au kaptura zaidi ya moja. g. Nywele ndefu, kunyoka kihuni, kuweka dawa nywele. h. Kufuga ndevu na kucha. i. Kuvaa mapambo.	Viboko visivyozi 6
15.	HESHIMA, UTII NA UAMINIFU	a. Mwanafunzi asiyesalimu walimu na yeyote anayemzidi umri. b. Asiyetii amri aliyopewa na mwalimu, kiongozi au mkubwa yeyote. c. Mwanafunzi mwongo, mmbea au asiyemwaminifu au mchonganishi.	Onyo kali na adhabu ya viboko visivyozi 6.
16.	FUJO NA KELELE	Fujo na kelele darasani, mstarini, bwenini, mikutanoni au eneo lolote la shule.	Adhabu ya mazoezi ya mwili na viboko.
17.	AFYA	a. Kula vyakula ovyo ovyo njiani au sehemu zisizoruhusiwa na shule, kutafuna tafuna ovyo darasani au ofisi ya walimu au mstarini, kutupa au kutookota uchafu unaomzunguka, kutovaa nadhifu. b. Kutupa tupa ovyo uchafu na kutosafisha sehemu aliyopangiwa.	Onyo na viboko visivyozi 4.
18.	KUMILIKI SIMU AU LINE YA SIMU	Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki simu, line au simu na line kwa pamoja akiwa shuleni au nyumbani.	Kufukuzwa shule mara moja.

NB:-

1. Adhabu zilizotajwa hapo juu hazihusishi adhabu za mazoezi ya viungo, kulima, kusafisha maeneo n.k. Adhabu zote zitatolewa kulingana na uzoefu wa mtu kufanya makosa. Kukiri kwake na kuomba msamaha au kukataa na usumbufu kwa mwalimu.
2. Makosa mengine yasiyotajwa hapo juu yatashughurikiwa na walimu kulingana na uzito wa kosa husika.

KARIBU SHULE YA SEKONDARI RUHUWIKO UPATE ELIMU BORA, MALEZI BORA NA NIDHAMU THABITI


 THE HEADMASTER
 RUHUWIKO SECONDARY SCHOOL
 P.O.Box 448
 SONGEA, RUVUMA